# Ofisi ya Taifa ya Takwimu

S. L. P 796 Simu: 255- (022) 2122722/3/4 Nukushi:+225 (022)2130852
Dar es Salaam,-TANZANIA Barua pepe: dg@nbs.go.tz


*Unapojibu tafadhali taja:*
Kumb Na: NBS/S.40/21/489

**YALIYOJITOKEZA**

Tarehe: 09 Juni, 2014

## FAHIRISI ZA BEI ZA TAIFA KWA MWEZI MEI, 2014

## Utangulizi

### Maana ya Fahirisi za Bei za Taifa

Fahirisi za Bei za Taifa ni kipimo kinachotumika kupima mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma mbalimbali zinazotumiwa na sampuli wakilishi ya kaya binafsi nchini Tanzania. Bei za bidhaa na huduma zipatazo 224 hukusanywa kila mwezi kwa kila mkoa nchini.

### Mizania mpya za bidhaa na huduma za jamii na kizio cha bei

Mizania ya Fahirisi za bei za Taifa zimetokana na matumizi ya kaya binafsi kutoka mikoa 21 ya Tanzania Bara. Mizania inajumuisha matumizi ya kaya zote binafsi kutoka mijini na vijijini yaliyotokana na Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya binafsi wa mwaka 2007. Kizio cha bei kinachotumika kutengeneza Fahirisi za Bei za Taifa ni cha mwezi Septemba 2010.

### Makundi ya bidhaa na huduma za jamii

Marejeo ya Fahirisi za Bei za Taifa yamefanyika kwa kufuata makundi yaliyokubalika Kimataifa yanayoitwa mchanganuo wa matumizi binafsi "Classification of Individual Consumption by Purpose (COICOP)". Fahirisi mpya za Bei inajumuisha makundi 12 ya mfumo wa COICOP pamoja na fahirisi za bei kwa makundi maalumu. Makundi hayo maalumu ni; 1) Vyakula na vinywaji baridi-vikijumuisha vyakula vinavyoliwa majumbani na mahotelini; 2) Nishati na Mafuta - kundi hili linajumuisha umeme na aina nyingine za nishati zinazotumika majumbani pamoja na petroli na dizeli; 3) Fahirisi za bidhaa na huduma zote za jamii isipokuwa vyakula na vinywaji baridi; 4) Fahirisi za huduma zote za jamii isipokuwa vyakula, vinywaji baridi, nishati na mafuta.

### Namna ya kukokotoa Fahirisi za Bei za Taifa

Maboresho yamefanyika kwenye ukokotoaji wa Fahirisi mpya za Bei za Taifa, ikiwa ni pamoja na kutumia wastani wa jiometria "geometric means" kwenye kukokotoa Fahirisi za Bei katika ngazi za mwanzo badala ya wastani wa kawaida "arithmetic mean", matumizi ya mfumo ulioboreshwa wa ukokotoaji pamoja na mfumo mzima wa kukusanya na kuchambua bei. Kanuni ya "modified Laspeyres index" inaendelea kutumika kukokotoa Fahirisi za Bei za Taifa katika ngazi ya makundi makubwa.

## MFUMUKO WA BEI KWA KIPIMO CHA MWAKA UMEONGEZEKA HADI ASILIMIA 6.5

### Jedwali Namba 1: Badiliko la Fahirisi za Bei za Taifa kwa Mwezi Mei, 2014 (Septemba, 2010 = 100)

| Na. | KUNDI (MAIN GROUP) | Mizania (Weight) | Mei-13 | Aprili-14 | Mei-14 | Badiliko la mwezi mmoja | Badiliko la miezi 12 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Vyakula na vinywaji baridi | 47.8 | 152.48 | 166.99 | 165.81 | -0.7 | 8.7 |
| 2 | Vinywaji vyenye kilevi na bidhaa za tumbaku | 3.3 | 133.18 | 141.65 | 141.95 | 0.2 | 6.6 |
| 3 | Mavazi ya nguo na viatu | 6.7 | 128.44 | 132.29 | 132.41 | 0.1 | 3.1 |
| 4 | Nishati, Maji na Makazi | 9.2 | 154.04 | 168.67 | 166.84 | -1.1 | 8.3 |
| 5 | Samani, vifaa vya nyumbani na ukarabati wa nyumba | 6.7 | 126.69 | 129.74 | 129.78 | 0.0 | 2.4 |
| 6 | Gharama za Afya | 0.9 | 108.10 | 111.96 | 112.04 | 0.1 | 3.6 |
| 7 | Usafirishaji | 9.5 | 123.68 | 126.34 | 126.57 | 0.2 | 2.3 |
| 8 | Mawasiliano | 2.1 | 95.96 | 96.71 | 96.63 | -0.1 | 0.7 |
| 9 | Utamaduni na Burudani | 1.3 | 112.54 | 113.24 | 113.25 | 0.0 | 0.6 |
| 10 | Elimu | 1.7 | 113.16 | 119.18 | 119.16 | 0.0 | 5.3 |
| 11 | Hoteli na Migahawa | 6.4 | 133.53 | 136.38 | 137.06 | 0.5 | 2.6 |
| 12 | Bidhaa na huduma nyinginezo | 4.5 | 119.87 | 128.90 | 129.78 | 0.7 | 8.3 |
| **JUMLA – FAHIRISI BIDHAA ZOTE** | | **100** | **140.76** | **150.50** | **149.89** | **-0.4** | **6.5** |
| **Makundi Mengine Teule** | | | | | | | |
| 1 | Vyakula—vikijumuisha vyakula vilivyoliwa nyumbani na mahotelini | 51.0 | 150.39 | 165.48 | 164.45 | -0.6 | 9.3 |
| 2 | Nishati na Mafuta—kundi hili linajumuisha umeme na aina nyingine za nishati zinazotumika nyumbani pamoja na petroli na dizeli | 5.7 | 172.51 | 191.93 | 188.97 | -1.5 | 9.5 |
| 3 | Fahirisi za bidhaa na huduma zote za jamii isipokuwa vyakula | 49.0 | 129.36 | 134.87 | 134.70 | -0.1 | 4.1 |
| 4 | Fahirisi na huduma zote za jamii Isipokuwa vyakula, nishati na mafuta | 43.3 | 122.87 | 126.99 | 127.21 | 0.2 | 3.5 |

Mfumuko wa Bei wa Taifa kwa kipimo cha mwaka unapima kiwango cha badiliko la kasi ya bei za bidhaa na huduma zote zinazotumiwa na kaya binafsi. Jedwali Namba 1 hapo juu linaonyesha kuwa, Mfumuko wa Bei wa Taifa kwa mwezi Mei, 2014 umeongezeka hadi asilimia 6.5 kutoka asilimia 6.3 ilivyokuwa mwezi Aprili, 2014. Hii inamaanisha kuwa, kasi ya upandaji wa bei za bidhaa na huduma kwa mwaka ulioishia mwezi Mei, 2014 imeongezeka ikilinganishwa na kasi iliyokuwepo kwa mwaka ulioishia mwezi Aprili, 2014. Fahirisi za Bei zimeongezeka hadi 149.89 kwa mwezi wa Mei, 2014 kutoka 140.76 mwezi Mei, 2013. Mfumuko wa Bei wa bidhaa za Vyakula na Vinywaji Baridi umeongezeka hadi asilimia 8.7 mwezi Mei, 2014 kutoka asilimia 7.8 ilivyokuwa mwezi Aprili, 2014.

### Mfumuko wa Bei kwa Bidhaa za Vyakula na Bidhaa Zisizo za Vyakula

Badiliko la Fahirisi za Bei za bidhaa za vyakula nyumbani na migahawani limeongezeka hadi asilimia 9.3 mwezi Mei, 2014 kutoka asilimia 8.5 mwezi Aprili, 2014. Badiliko la Fahirisi za Bei kwa


bidhaa zisizo za vyakula limepungua hadi asilimia 4.1 mwezi Mei, 2014 kutoka asilimia 4.9 mwezi Aprili, 2014.

## Mfumuko wa Bei wa Bidhaa na Huduma Zote Isipokuwa Bidhaa za Vyakula na Nishati

Aina hii ya Fahirisi haijumuishi vyakula vilivyoliwa nyumbani na migahawani, vinywaji baridi, petroli, dizeli, gesi ya kupikia, mafuta ya taa, mkaa na umeme. Vyakula na nishati vina sifa ya kuwa na bei ambazo hubadilika mara kwa mara hivyo vikiondolewa kwenye Fahirisi ya bidhaa na huduma zote hubakia Fahirisi ambayo ina mwelekeo imara kwa Watunga Sera.

Mfumuko wa Bei ambao haujumuishi vyakula na nishati kwa mwezi wa Mei, 2014 umepungua hadi asilimia 3.5 ikilinganishwa na asilimia 4.3 mwezi Aprili, 2014.

**Kielelezo Namba 1: Mwenendo wa Fahirisi za Bei za Taifa na Mfumuko wa Bei Kutoka Mei, 2013 Hadi Mei, 2014. (Septemba 2010 = 100)**




Kielelezo Namba 1 hapo juu kinaonyesha kuwa, katika kipindi cha kati ya mwezi Mei, 2013 hadi Mei, 2014, Fahirisi za Bei zimeonyesha mwenendo imara kutoka mwezi Mei, 2013 hadi Septemba, 2013. Lakini, Fahirisi za Bei zimekuwa na mwenendo wa kuongezeka kutoka mwezi Oktoba, 2013 hadi mwezi Mei, 2014. Mfumuko wa Bei umekuwa na mwenendo wa kushuka kutoka asilimia 8.3 mwezi Mei, 2013 hadi kufikia asilimia 6.5 mwezi Mei, 2014.

## MFUMUKO WA BEI KWA KIPIMO CHA MWEZI UMEPUNGUA KWA ASILIMIA 0.4

Mfumuko wa Bei wa mwezi Mei, 2014 unaopimwa kwa kipimo cha mwezi umepungua kwa asilimia 0.4 ikilinganishwa na ongezeko la asilimia 0.7 kama ilivyokuwa mwezi Aprili, 2014. Fahirisi za Bei zimepungua hadi 149.89 mwezi Mei, 2014 kutoka 150.50 mwezi Aprili, 2014. Kupungua kwa fahirisi kumechangiwa na kupungua kwa bei za bidhaa za vyakula na bidhaa zisizo za vyakula. Baadhi ya bidhaa za vyakula zilizochangia kupungua kwa fahirisi ni pamoja na; mahindi kwa asilimia 4.9, unga wa muhogo kwa asilimia 2.9, dagaa wakavu kwa asilimia 3.5, samaki wakavu kwa asilimia 6.2, matunda jamii ya machungwa kwa asilimia 5.6, nazi kwa asilimia 2.8 na

mbogamboga kwa asilimia 2.3. Kwa upande mwingine, bei za bidhaa zisizo za vyakula zilizochangia kwa kiasi kikubwa kupungua kwa fahirisi ni pamoja na bei za mkaa kwa asilimia 2.6 na bei za gesi ya kupikia kwa asilimia 1.3.


## Thamani ya Shilingi ya Tanzania Mwezi Mei, 2014 Ikilinganishwa na Mwezi Septemba, 2010

**Tafsiri**: Thamani ya Shilingi ya Tanzania inatafsiriwa kuwa ni badiliko la Uwezo wa Shilingi ya Tanzania katika kununua bidhaa na huduma zilezile za mlaji ambazo Shilingi ya Tanzania ingeweza kununua katika vipindi tofauti. Ikiwa wastani wa Fahirisi za Bei za Taifa unaongezeka, Uwezo wa Shilingi ya Tanzania katika kununua bidhaa na huduma hupungua.

Uwezo wa Shilingi 100 ya Tanzania katika kununua bidhaa na huduma umepungua hadi Shilingi 66 na senti 72 mwezi Mei, 2014 kutoka mwezi Septemba, 2010.

## MIENENDO YA BEI

### Kielelezo Namba 2: Mienendo ya Bei kwa Makundi Mbalimbali ya Fahirisi za Bei Kutoka Mei, 2013 hadi Mei, 2014. (Septemba 2010 = 100)




Kielelezo Namba 2 hapo juu kinaonesha mienendo ya bei kwa makundi mbalimbali ya Fahirisi za Bei kuanzia mwezi Mei, 2013 hadi mwezi Mei, 2014. Kwa wastani, Fahirisi za nishati na mafuta na Fahirisi za vyakula na vinywaji baridi zimekuwa na mwenendo wa juu kwa kipindi chote zikilinganishwa na fahirisi nyingine. Kundi la nishati na mafuta limeonyesha pia kuwa na mwenendo wa fahirisi usio imara ikilinganishwa na makundi mengine kwa kipindi husika. Fahirisi za bidhaa zisizo za chakula na fahirisi za bidhaa zisizo jumuisha chakula pamoja na nishati zimeonesha mwenendo wa bei ulio imara.

**Mawasiliano: Mkurugenzi Mkuu,**
**Ofisi ya Taifa ya Takwimu**